



## MAJIBU YA MASWALI? YAKO!

**Je, usafiri utatolewa kwa mtoto wangu hadi shule mpya waliopangiwa?**

**Ndiyo**, usafiri utatolewa kwa wanafunzi wanaohudhuria shule mpya waliyopangiwa. Usafiri pia utatolewa kuitia mfumo wa kituo cha chaguo kwa wanafunzi ambao wamekubaliwa kuijunga na Shule ya SAISD Choice. **Hakuna** uhakikisho wa usafiri kwa wanafunzi wanaochagua kuhudhuria shule tofauti ya mtaani ya SAID.

**Je, nina chaguo zipi za kujiandikisha kwa mwaka wa masomo wa 24-25?**

SAISD inathamini maoni na chaguo za wanafunzi na familia. Familia zimepewa uwezo wa kuchagua shule inayokidhi mahitaji ya mtoto wao vyema zaidi. Kila familia itapewa shule mpya ya nyumbani inayopendekezwa na wilaya; wanaweza pia kufuata chaguo za uandikishaji wa mwanafunzi (zinazoonyeshwa upande wa kulia)

**Je, mchakato huu utakuwa rahisi kwangu wakati wa mpito?**

Tumejitolea kutoa usaidizi wa moja kwa moja kwa familia ili kuhakikisha mabadiliko ya haraka kwa shule mpya, ikiwa ni pamoa na kukamilisha uandikishaji wa wanafunzi baada ya wao kuonyesha mapendeleo kwenye utafiti wa mapendeleo.

**Ninahitajika kutoa hati gani katika shule mpya ya nyumbani ili niweze kumwandikisha mtoto wangu?**

Hati mpya **hazitahitajika**. Taarifa za mwanafunzi wa SAISD zitahamishiwa kiotomatiki hadi shule mpya waliopangiwa. Familia itahitaji kujaza utafiti wa mapendeleo na kukamilisha usajili katika mfumo wa uandikishaji.

**Je, mtoto wangu atapewa kipaumbele cha kuhudhuria shule ya SAISD Choice ikiwa hilo ndilo chaguo ninalochagua?**

**Ndiyo**, ikiwa familia inatuma ombi la kuijunga na shule ya Choice, itapata fursa ya kuorodhesha kwa mpangilio shule zote ambazo wangependa kuhudhuria. Mfumo wa uandikishaji wa Wilaya utatoa nafasi katika shule iliyoorodheshwaa juu kabisa ambayo ombi hilo linastahiki na ambayo ina nafasi kwa ajili yao.

## CHAGUO ZA UANDIKISHAJI ZA WANAFUNZI

Kila familia itapewa shule mpya ya nyumbani, inayopendekezwa na Wilaya. Familia pia zinaweza kuchagua kutoka kwa chaguo zilizo hapa chini ili kupata shule zinazofaa zaidi.

### Chaguo la 1 WILAYA INASAJILI

Familia inachagua **kuhudhuria shule mpya ya nyumbani iliopangiwa**.

**USAFIRI UNATOLEWA**

### Chaguo la 2 MZAIZI ANATUMA OMBI

Familia inachagua **kutohudhuria shule mpya iliopangiwa ya nyumbani na inatuma ombi la mpango wa SAISD Choice/magnet wakati wa kipindi cha kutuma maombi** (tarehe 1 Des hadi 15 Feb).

**USAFIRI UNATOLEWA**

### Chaguo la 3 MZAIZI ANAOMBA UHAMISHO

Familia inachagua **kutohudhuria shule mpya ya nyumbani au chaguo la shule ya Choice na inachagua kuhudhuria shule tofauti ya SAISD**.

**HAKUNA HAKIKISHO LA USAFIRI**

## WASILIANA NASI

**SIMU YA DHARURA YA EMPOWER FAMILY**  
(210) 244-0845 | [empowerfamilies@saisd.net](mailto:empowerfamilies@saisd.net)

**OFISI YA USAJILI WA SAISD**  
(210) 554-2660

**UNGANA NASI KWENYE  
MIKUTANO YETU YA MTAANI**  
Changanua Msimbo wa QR ili kuona kalenda



Tembelea tovuti ya Rightizing ili kuona Mpango mzima wa Mpito wa Empower  
[WWW.SAID.NET/RIGHTSIZING](http://WWW.SAID.NET/RIGHTSIZING)